

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Simu: 023 2010199  
Kipepesi: 023 20111338  
Barua pepe  
[ded.mafia@pwani.go.tz](mailto:ded.mafia@pwani.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji  
P. O Box 85  
**MAFIA.**

**Kumb Na. MDC/S.20/5/VOL.II/47**

**15/3/2019**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi ya kazi kama ifuatavyo:-

**1. MKATISHAJI WA TIKETI ZA BOTI (NAFASI 2)**

**1.1 SIFA ZA MWOMBAJI:**

Mwombaji awe amehitimu Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) na kuhitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo Masoko (Marketing) huduma kwa wateja (Customer Service), Usimamizi wa Biashara( Business Administration), kutoka Chuo chochote kinacho tambuliwa na Serikali.

Awe anajua kuongea,kusoma na kuandika Kiswahili na Kingereza kwa ufasaha

Awe anajua kutumia Kompyuta

**1.2 MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia viwango vya Mishahara yaani **TGS B1 sawa na TSH 390,000**

### **1.3 KAZI ZA KUFANYA**

- i. Kukatisha tiketi kwa abiria wanaosafiri kwa boti ya serikari kutoka Mafia-Nyamisati-Dar na Nyamisati-Mafia-Dar
- ii. Kuandaa kumbukumbu za Abiria wote wanaosafiri kila siku na kuwasilisha kwa mamlaka husika
- iii. Kuhakikisha abiria wote wanaosafiri wamekata tiketi na kufanya malipo kabla ya safari
- iv. Kuwaongoza abiria kupanda na kushuka kwenye meli na kuhakikisha kila abiria amekaa sehemu husika kabla ya meli kuruhusiwa
- v. Kuwasilisha fedha za mauzo ya tiketi Benki kila siku baada ya kufunga mauzo

### **1.4 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.**

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
- ii. Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- iii. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayo jitosheleza (detailed CV) yenye anuani na namba za simu pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu(3) wa kuaminika
- iv. Maombi yote yaambatane na barua ya maombi iliyoandikwa kwa mkono. nakala ya vyeti vya taaluma, nakala ya vyeti vya kidato cha Nne au Sita kwa walio fikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- v. Waombaji waambatanishe picha mbili za passport size za hivi karibuni
- vi. Testimonials , Provisional results, statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita havita kubaliwa

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 22/3/2019**

Maombi yote yawasilishwe masijala kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) au kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (w)**  
**Halmashauri ya Wilaya Mafia**  
**S.L.P 85**  
**MAFIA**

Imetolewa na



.....  
**ERICK C. MAPUNDA**  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**MAFIA**

